

Dhambi Inakuotea Mlangoni

na

Terry Warford

Dhambi Inakuotea Mlangoni

na

Terry Warford

Novemba 6, 2011

Dhambi Inakuotea Mlangoni

Moja ya changamoto tunayokumbana nayo kama Wakristo ni ujirani wa dhambi. Inaonekana na maranyingi ipo karibu na sisi.

Kaini alichukia katika sura ya 4 ya Mwanzo kwa sababu dhabihu ya Abeli ili kubaliwa na Mungu na Kaini kukataliwa. Mungu alimuonya ni jinsi gani dhambi ilikuwa karibu naye. Mwanzo 4:7, *“Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo ianakutamani wewe, walakini yapasaa uishinde.”*

Msitari huu hauonyeshi tu kuwa karibu na dhambi, bali pia suluhisho. Ni rahisi, kuna sehemu 4 ya somo kwetu sisi, sehemu 2 ya maonyo, na sehemu 2 ya tumaini. Natarajia tunaweza kujifunza somo hili kirahisi kuliko Kaini alivyofanya.

Tutaangalia sehemu hizi 4 katika mtiririko wa msitari, ili kwamba tuweze kuanza na tatizo, na kumalizia na suluhisho.

“Dhambi imelala mlangoni”

Changamoto muhimu tunayoangalia ni jinsi gain dhambi ipo karibu na sisi.

Ebr. 12:1, *“Basin a sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu.”*

Sababu moja ambayo inasababisha dhambi kuturudisha nyuma kirahisi ni kwamba Shetani anatushambulia kwa karibu, anatushadhaifisha, kwa hali ya wingi zaidi. 1 Yoh. 2:16, *“Maana kila kilichomo duniani, yaani, tama ya mwili, na tama ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na baba, bali vyatokana na dunia.”* Miili yetu, macho na moyo vipo karibu na sisi, na hupatikana kwa ajili ya silaha za Shetani.

Hivyo, tunaruhusuje dhambi kuwa karibu na sisi?

“Kama haufanyi vyema, dhambi inalala mlangoni.”

Kimsingi, tunaruhusu dhambi kuwepo karibu na sisi tunapokuwa karibu na dhambi. Tunaweza kutumia somo hili katika njia mbili tofauti, vyote kwa usahihi.

Kwanza, kama hatufanyi vyema, kama sio kufanya matendo mema, dhambi inalala mlangoni. Yakobo 4:17, *“Hivyo basi ye yote ajuaye kutenda mema na asitende, huyo kwake ni dhambi.”*

Pili, kama hatufanyi vyema, kama kufanya matendo mabaya, dhambi inalala mlangoni. 1 Yoh. 3:4, *“Kila atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi.”* Pia tunaweza kujikuta sisi wenyewe karibu na dhambi kwa kusukuma furushi la mema na mabaya.

1 Yoh. 5:17, *“Kila lisilo la haki ni dhambi, na dhambi iko isiyo ya mauti.”*

Sasa tunataka kuwa na hakika kwamba vitu tuvifanyavyo vinampendeza Mungu.

Efe. 5:10, *“Mkihakiki ni nini impendezayo Bwana.”*

Na kwa kadiri tuwezavyo tunataka kuepuka uovu. Hatuwezi kuepuka majaribu kabisa. Lakini kama tukiepuka tukiwezacho, inaifanya kuwa rahisi kushinda kile kinachokuja katika njia yetu. 1 Pet. 3:10-11, *“Kwa maana atakaye kupenda maisha, na kuona siku njema, auzuie ulimi wake usinene mabaya, na midomo yake isinene hila. Na aache mabaya, atende mema; atafute amani aifuata sana.”*

“Hautakubaliwa?”

Ndiyo tunaweza kukubaliwa na Mungu siku ya hukumu, kama mtumishi mwenye faida katika Math. 25:21, *“Bwana wake akamwambia, vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.”*

Na kama tukikubaliwa tutaishi pamoja Naye milele Mbinguni. Yesu alisema katika Ufu. 3:21, *“Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.”*

Tuna hakikishaje kwamba tutakubaliwa?

“Kama ukifanya vyema, hautakubaliwa?”

Kwa nini mtumishi mwenye faida aliambiwa na bwana wake “umefanya vyema”? Kwa urahisi, alimwambia “umefanya vyema” kwa sababu alifanya vyema. Math. 25:20-21, *“Akaja yule aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema, Bwana, uliweka kwangu talanta tano; tazama talanta nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, vema mtumwa mwema na mwaminifu, ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.”*

Matendo yetu mema hufanya imani yetu kukomaa. Ebr. 4:11, “*Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*”

Na tutazawadiwa kulingana na matendo yetu, Math. 16: 27, “*Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa baba yake pamoja na malaika zake; ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.*”

Hivyo, somo la sehemu 4 kutoka katika Mwanzo 4:7 ni rahisi, na pia ni muhimu sana. “*Kama ukifanya vyema, hautakubaliwa? Na kama haukufanya vyema, dhambi inalala mlangoni.*”

Katika upendo wa Mkristo

Ndg. Terry Warford

